# HOTUBA FUPI YA MGENI RASMI,MH.MKUU WA MKOA WA RUKWA KATIKA ZOEZI LA UGAWAJI WA VIFAA VYA HUDUMA ZA UZAZI VILIVYOTOLEWA NA MHESHIMIWA RAIS KATIKA MKOA WA RUKWA TAREHE 27 JULAI 2017

- Katibu Tawala wa Mkoa
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Rukwa
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya
- Waheshimiwa Wabunge
- Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri
- Mganga Mkuu wa Mkoa
- Wajumbe wa sekretarieti ya Mkoa na wataalam wote kutoka Ofisi ya Mkoa
- Makatibu Tawala wa Wilaya
- Wakurugenzi wa Halmashauri
- Waganga Wakuu wa Halmashauri
- Mwenyekiti wa Bodi ya Afya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga

- Wajumbe wa kamati ya uendeshaji wa huduma katika kituo cha Afya Mazwi
- Wataalamu wote kutoka ngazi ya Wilaya na taasisi
- Waandishi wa habari
- **Mabibi na mabwana**

Kwanza naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote mliofika kwa ajili ya kunisikiliza na kushuhudia tukio hili muhimu la kupokea zawadi kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wote aliotuteua tumuwakilishe, amekuwa akionyesha moyo na nia ya dhati ya kuhakikisha tunapambana na changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya afya.

Ninatambua kwamba tuna changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya afya hususani upungufu wa vifaa muhimu vinavyohitajika katika kutoa huduma bora za afya hapa nchini na katika Mikoa yetu.

Katika juhudi za kumaliza changamoto hii, Serikali ya awamu ya tano kupitia kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Jonh Pombe Joseph Magufuli iliamua kuchukua uamuzi wa kununua vifaa vya kutosha vya huduma za uzazi kupitia bohari kuu ya dawa (MSD) kwa ajili ya kuvigawa katika Halmashauri zote Nchini ikiwa ni pamoja na Halmashauri za Mkoa wa Rukwa.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Vifaa ambavyo vimetolewa na Mheshimiwa Rais na ambavyo nimevikagua, ni vitanda vinavyotumiwa na akina mama wakati wa kujifungua, vitanda vya hospitali, magodoro na mashuka. Nimeambiwa kuwa kwa ujumla Mkoa umepata.

(i) Vitanda 16 vyakuzalishia,

(ii) Vitanda 80 vya Wagonjwa,

(iii) Magodoro 80, na

(iv) Mashuka 200.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Idadi kama hii ya vifaa pia imetolewa katika Halmashauri zote nchini. Kwa hiyo mnaweza kuona ni gharama kubwa kiasi gani iliyotumiwa na Serikali kununua vifaa hivi kwa lengo la kuboresha huduma za uzazi nchini. Ndio maana Mheshimiwa Rais amesisitiza sana watu tulipe kodi wote ili kutatua kero mbalimbali za wananchi hususan watu wa hali ya chini. Nataka nisisitize ulipaji wa kodi ili kazi kama hii na zingine zifanyike.

Wito wangu kwa viongozi wote mlioko hapa ni kuhakikisha vifaa hivi vinafikishwa katika vituo vyetu hususani vituo vyenye upungufu mkubwa ili

wananchi wanufaike na juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Kwa watumishi na viongozi wa sekta ya afya ni wajibu wenu kuhakikisha vifaa hivi vinatunzwa vizuri na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuanzia sasa sitegemei kusikia kwamba ndani ya Mkoa wangu kuna mahali mama mjamzito analala chini au amejifungulia chini.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Nimeona Kituo hiki cha Afya Mazwi kimeanza kutoa huduma za kujifungua. Waliohusika kuwezesha mama Wajawazito kuondokana na usumbufu wa kutafuta huduma hii mbali na maeneo yao kwa muda mrefu. Ningependa kuona mnaendelea kuwa wabunifu na sehemu zingine kama hii ili kupunguza adha zinazotokea kwa mama wajawazito.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Nimejionea mwenyewe akinamama kadhaa tayari wameanza kupata huduma za kujifungua na kuanzia mlipoanza kutoa huduma hizi mnamo tarehe 01 Julai 2017 hadi leo tayari jumla ya akinamama zaidi ya 20 wamejifungulia hapa.Nawapongeza watumishi wote wa kituo hiki kwa kuitikia kutekeleza maelekezo haya muhimu ya Kisera ya kuhakikisha mama wajawazito wanajifungulia katika kituo hiki.

Maelekezo yangu katika hili ni kuhakikisha kwamba, huduma za uzazi na mtoto zinatolewa bila malipo yoyote. Sera yetu ya afya ya mwaka 2007 inataka makundi maalumu zikiwemo huduma za uzazi na huduma za afya kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 zitolewe bila malipo yoyote ikiwa ni pamoja na kutowataka watu hawa kwenda kununua dawa na vifaa vya kujifungulia kutoka nje ya vituo vyetu

**Ndugu Katibu Tawala,**

Kwa upande wa wananchi niwaombe watambue kwamba Serikali ya Mkoa iko makini katika kuhakikisha akinamama na wananchi wote kwa ujumla wanapata huduma za afya zinazostahili. Natoa wito sasa kuanzia sasa akina mama wajawazito wote wanaotoka maeneo ya jirani. Na kituo hiki wanapofikia muda wa kuanza kliniki, waje katika kituo hiki. Wanapofikia siku za kujifungua waanzie katika kituo hiki ili kuwapa nafasi nzuri wataalamu wetu katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa kutoa huduma za rufaa na huduma za kibingwa kwa wale wanaopewa rufaa ya kwenda hospitali ya Mkoa.

Bahati nzuri kituo hiki kipo jirani na Hospitali ya Mkoa. Iwapo wataalamu katika kituo hiki watabaini kuwa mama hawezi kujifungulia katika kituo hiki kutokana na sababu mbalimbali, itakuwa rahisi kumpeleka katika hospitali yetu ya Mkoa.

Katika hili nisingependa kusikia kuwepo kwa changamoto ya usafiri kwa kuwa hapa ni jirani,ni vyema magari ya kusafirisha wagonjwa yaliyopo katika hospitali ya Mkoa yatumike kufanya kazi ya kubeba wagonjwa kutoka katika kituo hiki ikibidi

**Ndugu Katibu Tawala,**

Ipo tabia kwa baadhi ya watumishi wa Afya kuwadhalilisha Mama Wajawazito wakati wa kujifungua. Nawataka waache tabia hiyo mara moja. Wafanye kazi yao kwa unyenyekevu sana na siku walipokuwa wakiomba kazi hiyo. Naagiza yoyote yule atakayekiuka maadili ya kazi atachukuliwa hatua pale pale na kuadhibiwa vilivyo.

**Ndugu Katibu Tawala,**

Niwapongeze pia kwa juhudi zenu za kuendelea na ukamilishaji wa jengo litakalowezesha huduma nyingine zinazohusiana na uzazi kuendelea kutolewa. Ni matumaini yangu kuwa litakamilika ndani ya muda mfupi kuanzia sasa.

Nina taarifa kwamba Serikali kuu kupitia OR-TAMISEMI, ina mkakati wa kuhakikisha vituo vyote vya afya nchini vinatoa huduma za upasuaji kwa akinamama wakati wa kujifungua na hata kituo hiki kutakiwa kupeleka makisio ya ujenzi wa jengo la upasuaji.

Natumia fursa hii kuwaagiza Wakurugenzi wote wa wa Halmashauri kuhakikisha wanaendelea kukamilisha miundombinu ya aina hii wakati tukiendelea kuwasiliana na ngazi za juu.

Napenda pia niwakumbushe wananchi wote muone umuhimu wa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya.

Mwisho napenda kutamka rasmi kwamba vifaa vya huduma za uzazi vilivyotolewa na Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa nimevigawa rasmi na huduma za kujifungua katika kituo cha afya Mazwi zimezinduliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

ZELOTE STEPHEN ZELOTE

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**